**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA KILIMO**

# MWONGOZO WA UENDESHAJI WA MIFUKO YA MAENDELEO KWENYE VYAMA VYA USHIRIKA

***Imeandaliwa na:***

Tume ya Maendeleo ya Ushirika

S. L. P 201,

**DODOMA**

***TOLEO LA KWANZA    APRIL, 2022***

# YALIYOMO

**YALIYOMO** ........ i
**DIBAJI** ........ ii
**UTANGULIZI** ........ iii
**SEHEMU YA KWANZA** ........ 1
**MADHUMUNI YA MWONGOZO** ........ 1
**SEHEMU YA PILI** ........ 1
**UANZISHAJI WA MFUKO WA MAENDELEO** ........ 1
**1.1. Taratibu za Uanzishaji wa Mfuko** ........ 1
**1.2. Uchangiaji wa Mfuko wa Maendeleo** ........ 2
**SEHEMU YA TATU** ........ 3
**USIMAMIZI WA MFUKO WA MAENDELEO** ........ 3
**3.1 Kamati ya usimamizi wa mfuko** ........ 3
**3.1.1Muundo wa Kamati ya Usimamizi** ........ 3
**3.1.2Upatikanaji wa Kamati ya Usimamizi** ........ 3
**3.1.3Wajibu wa Kamati ya Usimamizi** ........ 3
**3.2 Majukumu ya Bodi ya Chama** ........ 4
**3.3 Matumizi ya Fedha za Mfuko** ........ 4
**3.4 Utunzaji wa Hesabu za Mfuko** ........ 5
**3.5 Taarifa za Hesabu za Mfuko** ........ 5
**SEHEMU YA NNE** ........ 7
**HITIMISHO** ........ 7


# DIBAJI

Mwongozo wa Uendeshaji wa Mifuko ya Maendeleo kwenye Vyama vya Ushirika ni muhtasari wa shughuli nzima ya uanzishwaji, uendelezwaji na uhifadhi wa Mifuko ya maendeleo kwenye Vyama vya Ushirika vya Msingi, Benki za ushirika, Vyama Vikuu vya ushirika, Miradi ya Pamoja ya Ushirika, Miradi ya Ubia na Shirikisho la Vyama vya Ushirika.

Mwongozo huu ambao umeandaliwa kwa mujibu wa Kifungu cha 142 (k) cha Sheria ya Vyama vya Ushirika, unafafanua taratibu za uanzishwaji, uchangiwaji, usimamizi, matumizi ya fedha za mfuko, sambamba na ukaguzi wake na uwasilishwaji wa taarifa za Hesabu za mfuko zilizokaguliwa kwenye Mikutano Mkuu na kuwasilishwa kwa Mrajis wa Vyama vya Ushirika.

Ninayo matumaini kuwa Mwongozo huu utavisaidia Vyama vya Ushirika katika upatikanaji wa fedha kwa ajili ya shughuli mbalimbali za maendeleo ya Vyama vya ushirika zikiwemo Uwekezaji katika maeneo mbalimbali, Masoko, ununuzi wa pembejeo zinazokidhi sifa na ubora wa uzalishaji wa mazao n.k. Mifuko hii itasaidia kupata fedha kwa njia rahisi na gharama nafuu ikilinganishwa na vyanzo vingine vya fedha.

Aidha, Mwongozo huu utaisaidia Ofisi ya Mrajis wa Vyama vya Ushirika kufanya ufuatiliaji na tathmini ya mipango pamoja na shughuli za maendeleo zinazofanywa kwenye Vyama vya Ushirika na kuona namna zinavyomnufaisha Mwanachama, Chama cha Ushirika na Taifa kwa ujumla.



Dkt. Benson O. Ndiege
**MRAJIS WA VYAMA VYA USHIRIKA**

## UTANGULIZI

Mwongozo wa uendeshaji wa mifuko ya maendeleo ni nyenzo inayotoa maelekezo ya namna ya kuanzisha na kuendesha mifuko ya maendeleo katika Vyama vya Ushirika vya msingi, vyama miradi ya pamoja ya Vyama vya Ushirika, Miradi ya ubia wa pamoja, benki za ushirika, Vyama Vikuu na Shirikisho la Vyama vya Ushirika; kwa malengo ya kugharimia shughuli mbalimbali za maendeleo ikiwa ni pamoja na Uwekezaji katika maeneo mbalimbali, Masoko, ununuzi wa pembejeo n.k. Mwongozo huu unaandaliwa kwa mujibu wa Kifungu Na. 142(k) cha Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2013.

Kumekuwa na changamoto mbalimbali kwenye uanzishwaji wa Mifuko ya Maendeleo kwenye Vyama vya Ushirika. Changamoto hizo ni pamoja na: Vyama kuanzisha mifuko isiyokuwa na utaratibu maalum; shughuli za mifuko kuingiliana na shughuli za kawaida za chama; mifuko inayoanzishwa kukosa usimamizi madhubuti na kufanya matumizi kinyume na malengo yaliyokusudiwa n.k.

Ili kutatua changamoto hizo, Ofisi ya Mrajis imetoa mwongozo huu ili kuvielekeza vyama mambo muhimu ya kuzingatia kabla na baada ya kuanzisha mfuko wa maendeleo, ili kufikia malengo tarajiwa na kuepusha matumizi mabaya ya fedha za mfuko.

Mwongozo huu umeandaliwa kwa lengo la kuweka uelewa wa pamoja kwenye vyama vyote vya ushirika ambavyo tayari vimeshaanzisha mifuko na vile ambavyo vinatarajia kuanzisha mifuko kwa ajili ya kutekeleza shughuli.

Mwongozo huu unatoa maelekezo mahsusi kwa ajili ya Bodi za Vyama vya Ushirika kuhusu namna ya uanzishwaji na uendeshwaji wa mifuko ya maendeleo ndani ya chama, baada ya kuonekana kuwa baadhi ya vyama vimekuwa vikianzisha mifuko hii bila kuwa na utaratibu maalum wa namna ya kuiendesha.

## SEHEMU YA KWANZA

## MADHUMUNI YA MWONGOZO

Madhumuni ya Mwongozo huu ni pamoja na:

(i) Kutoa utaratibu wa uanzishwaji na usimamizi wa mifuko ya maendeleo katika vyama vya ushirika;
(ii) Kuainisha malengo ya uanzishwaji wa mifuko ya maendeleo katika Vyama vya Ushirika; na
(iii) Kutoa maelekezo ya namna ya kukusanya fedha za mfuko.

## SEHEMU YA PILI

**UANZISHAJI WA MFUKO WA MAENDELEO**Chama cha Ushirika kinaweza kuanzisha mfuko wa maendeleo kutegemeana na mahitaji. Ili kuhakikisha kuwa mahitaji yaliyokusudiwa yanafikiwa, chama kinatakiwa kuzingatia taratibu wakati wa uanzishaji na uchangiaji wa mifuko hiyo kwa kuzingatia: taratibu za uanzishaji wa mfuko; na uchangiaji wa mfuko wa maendeleo.

### 1.1. Taratibu za Uanzishaji wa Mfuko

Uanzishwaji wa mfuko wa maendeleo katika chama cha ushirika utasimamiwa na Bodi ya chama ambapo itapaswa kuzingatia taratibu zifuatazo:

(i) Kufanya upembuzi utakaoainisha mahitaji na kuandaa mapendekezo ya kuanzishwa kwa mfuko;
(ii) Kupeleka mapendekezo kwenye Mkutano Mkuu kwa ajili ya kujadiliwa na kuazimia uanzishaji wa mfuko;
(iii) Endapo Mkutano Mkuu utapitisha mapendekezo hayo, Bodi ya chama itaandaa andiko kwa ajili ya uanzishwaji wa mfuko; na kisha
(iv) Kuwasilisha andiko la mfuko kwa Mrajis wa Vyama vya Ushirika kwa ajili ya kuidhinishwa.

## 1.2. Uchangiaji wa Mfuko wa Maendeleo

Uchangiaji wa mfuko wa maendeleo utategemeana na aina na mahitaji ya chama. Utaratibu wa uchangiaji wa mfuko wa maendeleo utakuwa kama ifuatavyo:

(i) Maamuzi ya namna ya kuchangia mfuko yatafanywa na wanachama katika Mkutano Mkuu. Chama hakitaruhusiwa kukusanya fedha pasipo ridhaa ya wanachama kwa kupitia Mkutano Mkuu**;**

(ii) Wanachama watajadili chanzo cha fedha, kiwango na muda watakaochangia kwenye mfuko kwa kuzingatia malengo ya uanzishwaji wa mfuko;

(iii) Fedha za mfuko zitachangwa kwa utaratibu uliokubaliwa kwenye Mkutano Mkuu ikiwa ni pamoja na; mwanachama kuchangia fedha taslimu, kukatwa kwenye mauzo ya mazao (kwa vyama vya mazao) na bidhaa/huduma nyingine; na

(iv) Fedha zilizochangwa kwenye mfuko hazitarudishwa kwa mwanachama, bali zitatumika kwa ajili ya malengo mahsusi yaliyoainishwa kwenye andiko la mfuko. Mwanachama atanufaika na mapato yatakayotokana na mfuko kwa kuzingatia uwiano wa kile alichochangia.

TANBIHI: Ni muhimu ikazingatiwa kwamba utaratibu wa makato kwa ajili ya shughuli za uanzishaji na uendeshaji wa mfuko hazitaongeza gharama za huduma kwa mwanachama kama vile makato kuingizwa kwenye gharama za pembejeo, n.k.

Mfuko utaendeshwa kwa mujibu wa malengo yaliyokusudiwa; hivyo, hautahusika katika kugharamia shughuli nyingine yoyote ambayo haikuwa kwenye lengo la uanzishwaji wake pasipo kupata idhini ya Mrajis wa Vyama vya Ushirika.

# SEHEMU YA TATU

# USIMAMIZI WA MFUKO WA MAENDELEO

Mfuko hauna budi kuwa na uongozi unaojitegemea ili kuondoa mwingiliano wa shughuli zake na zile za msingi za chama ikiwa ni pamoja na kuleta ufanisi na kuimarisha udhibiti wa shughuli za maendeleo ndani ya chama. Chama kitaunda kamati ambayo itakuwa na wajibu wa kusimamia shughuli za mfuko. Kamati hii itajulikana kama Kamati ya Usimamizi wa Mfuko.

## 3.1 Kamati ya usimamizi wa mfuko

Bila kuathiri majukumu ya kawaida ya Bodi ya Chama, Kamati ya Usimamizi wa Mfuko itafanya kazi zake za usimamizi wa shughuli zote za mfuko wa maendeleo kwa mujibu wa majukumu kama yalivyoainishwa kwenye Mwongozo huu.

### 3.1.1 Muundo wa Kamati ya Usimamizi

Kamati ya Usimamizi itaundwa na:

(i) Wajumbe wasiopungua wawili (2) ambao watatokana na wajumbe wa Bodi;
(ii) Mjumbe mmoja (1) kutoka nje ya Bodi ambaye atatakiwa kuwa na utaalam wa shughuli inayotarajiwa kufanyika; na
(iii) Mtendaji maalum kwa ajili ya kutunza vitabu na kumbukumbu zote za Mfuko.

### 3.1.2 Upatikanaji wa Kamati ya Usimamizi

Bodi ya Chama itapeleka mependekezo ya Wajumbe kwenye Mkutano Mkuu kwa ajili ya kuidhinishwa.

### 3.1.3 Wajibu wa Kamati ya Usimamizi

Kamati ya Usimamizi wa Mfuko itakuwa na Wajibu kama ifuatavyo:

(i) Kutoa mapendekezo kwenye Bodi kuhusu uendeshaji wa Mfuko;

(ii) Kuhamasisha uchangiaji wa mfuko na kuchukua hatua kwa mwanachama atakayekaidi maamuzi ya Mkutano Mkuu juu ya uchangiaji wa mfuko wa maendeleo kwa kushirikiana na Bodi ya Chama,;
(iii) Kutoa taarifa za uendeshaji wa mfuko katika vikao vya Bodi, Mkutano Mkuu wa Chama na katika ofisi ya Mrajis wa vyama vya Ushirika pale itakapohitajika;
(iv) Kusimamia rasilimali zote za mfuko, kwa kushirikiana na Bodi; na
(v) Kutekeleza shughuli zozote zile kwa ajili ya manufaa na maendeleo mfuko.

## 3.2 Majukumu ya Bodi ya Chama

Bodi, kama Msimamizi Mkuu wa shughuli za Chama, itatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Masharti ya Vyama vya Ushirika. Kwa upande wa Mfuko wa Maendeleo wa Chama, Bodi itakuwa na majukumu yafuatayo:

(i) Kuhakikisha kuwa Kamati ya Usimamizi wa Mfuko inatekeleza majukumu yake;
(ii) Kuhakikisha kuwa Kamati ya usimamizi inaandaa na kutunza taarifa za Mfuko;
(iii) Kusimamia na kudhibiti matumizi ya fedha za mfuko; na
(iv) Kuhakikisha kuwa malengo ya uanzishwaji wa Mfuko yanafikiwa.

Pale ambapo Bodi itaona kuwa Kamati ya Usimamizi imeshindwa kutekeleza majukumu yake, itapeleka mapendekezo kwenye Mkutano Mkuu kwa ajili ya maamuzi. Kutapokuwa na viashiria vya hatari katika uendeshwaji wa Mfuko, Mrajis wa Vyama vya Ushirika ataweza kuchukua hatua wakati wowote.

## 3.3 Matumizi ya Fedha za Mfuko

Matumizi yoyote za fedha za Mfuko yatafanyika kwa kuzingatia madhumuni yaliyoainishwa kwenye andiko la Mfuko. Ili kuimarisha udhibiti wa uendeshaji wa mfuko huo mambo yafuatayo yatatakiwa kuzingatiwa:

(i) Matumizi yoyote ya mfuko wa maendeleo ya chama yatafanyika baada ya kuwa yamepitishwa kwenye Mkutano Mkuu na kuidhinishwa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika.
(ii) Fedha za Mfuko zitakazohusu ununuzi wa vifaa au pembejeo zitatumika kwa kuzingatia taratibu za manunuzi zilizoelezwa kwenye sera/kanuni za manunuzi ya chama; na
(iii) Kufanya malipo ya fedha kwa mujibu wa taratibu za Kihasibu.

## 3.4 Utunzaji wa Hesabu za Mfuko

Ili kuhakikisha kuwa hakuna muingiliano wa fedha za chama, yafuatayo yanapaswa kuzingatiwa:

(i) Fedha za mfuko wa maendeleo zinapaswa kuwa na vitabu vyake maalum kwa ajili ya miamala ambayo hesabu zake zitaandikwa na kutunzwa kikamilifu;
(ii) Fedha za mfuko zitajitegemea na zitatakiwa kutunzwa katika akaunti maalum inayojitegemea;
(iii) Matumizi ya fedha za mfuko yatakaguliwa kwa utaratibu wa kawaida wa ukaguzi wa hesabu za chama. Mrajis wa Vyama vya Ushirika atakagua shughuli za mfuko wakati wowote kwa jinsi atakavyoona inafaa; na
(iv) Mkaguzi wa nje anayekagua hesabu za chama ndiye atayekagua hesabu za mfuko na taarifa yake itapelekwa kwenye Vikao vya Bodi, Mkutano Mkuu na katika ofisi ya Mrajis wa Vyama vya Ushirika.

## 3.5 Taarifa za Hesabu za Mfuko

(i) Taarifa za hesabu za mfuko zitawasilishwa katika vikao vya Bodi, na kisha kupelekwa kwenye Mkutano Mkuu ili wanachama waweze kujua mwenendo wa uendeshaji wa mfuko; na
(ii) Taarifa za fedha za mfuko zitaingizwa kwenye vitabu vya hesabu kwa utaratibu wa kawaida wa utunzaji wa hesabu za chama. Taarifa zinazopaswa kuandaliwa ni pamoja na;
    - Taarifa ya makusanyo ya fedha za Mfuko,

- Matumizi yaliyofanyika kupitia fedha za mfuko kulingana na bajeti iliyoidhinishwa, na
- Taarifa ya jumla ya mapato na matumizi ya fedha za mfuko.

**Tanbihi:** Mwongozo wa uendeshaji wa Mfuko wa Maendeleo utakaokuwa umeandaliwa na chama na kupitishwa na Mkutano Mkuu wa Chama husika utapaswa kusajiliwa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika.

Aidha, Usimamizi na udhibiti wa utekelezaji wa Mwongozo huu utafanywa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania.

## SEHEMU YA NNE

## HITIMISHO

Mifuko ya maendeleo katika Vyama vya Ushirika itachangia katika maendeleo ya vyama husika endapo itatumika kwa kuzingatia madhumuni ya uanzishwaji wake. Hata hivyo; katika baadhi ya Vyama ambavyo vimekwishaanzisha Mifuko hii, kumekuwa na changamoto mbalimbali zilizosababisha kuzorota/kutofikiwa kwa malengo ya uanzishwaji wa mifuko hiyo.

Mwongozo huu utasaidia kutatua changamoto zilizopo katika uanzishaji, uendeshaji na usimamizi wa Mifuko hii muhimu katika Vyama vya Ushirik,a iwapo kila Mdau atatekeleza wajibu wake.

Vilevile, utekelezaji wa mwongozo huu utavisaidia Vyama vya Ushirika ambavyo tayari vimekwishaanzisha mifuko ya maendeleo ambayo imekuwa na changamoto nyingi vingi viweze kufanya kazi vizuri. Kwa kutumia Mwongozo huu, Mrajis wa Vyama vya Ushirika atakuwa na nafasi nzuri ya kusimamia Mifuko hii ili iweze kuwa na tija na kuvisaidia Vyama vya Ushirika kuondokana na utegemezi kutoka kwenye Taasisi mbalimbali za kifedha.